# Ripoti zilizoandikiwa kwa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya ziada au lahaja kwa K-10

## Taarifa kwa wazazi na walezi

Wapendwa wazazi na walezi

Huwa unapokea ripoti mbili zilizoandikiwa kutoka shule ya mtoto wako kila mwaka. Ripoti hizi zitakusaidia kuelewa jinsi ya mtoto wako anavyoendelea na jinsi ya shule yako inavyosaidia mtoto wako kujifunza. Kila ripoti itaonyesha maendeleo katika masomo yote.

### Ripoti kwa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya ziada au lahaja (English as an additional language or dialect (EAL/D))

Iwapo mtoto wako anajifunza Kiingereza kama lugha ya ziada au lahaja (EAL/D), ripoti itaeleza jinsi ya maendeleo yao ya lugha ya Kiingereza yalivyosaidiwa na maendeleo ya mtoto wako katika kujifunza lugha ya Kiingereza. Kwa wanafunzi wa mwaka wa 1 na kupanda juu ripoti itajumuisha pia awamu yao ya sasa ya ustadi wa lugha ya Kiingereza. Awamu zinaitwa kuanza, kujitokeza, kuendelea au kuimarika. Tafadhali tazama upande mwingine wa ukurasa huu kwa maelezo ya awamu hizi.

### Ripoti kwa wanafunzi wapya waliowasili wa (EAL/D)

Iwapo mtoto wako yupo kwenye mpango wa EAL/D na amekuwepo katika shule ya Australia kwa muda wa vipindi vinne au chini ya hivi, ripoti iliyoandikiwa ya mtoto wako inaweza kujumuisha maoni kuhusu maendeleo yao katika masomo wanayojifunza badala ya daraja.

### Ripoti kwa wanafunzi wapya waliowasili wa EAL/D katika Vituo vya Kiingereza Makini au Shule ya Juu ya Kiingereza Makini

Iwapo mtoto wako amejiandikisha katika Kituo cha Kiingereza Makini au Shule ya Juu ya Kiingereza Makini, utapokea ripoti iliyoandikiwa kuhusu maendeleo yao ya kujifunza Kiingereza. Aidha, ripoti itaonyesha maendeleo katika masomo yote yaliyosomwa katika maandalizi ya shule ya juu.

| Awamu za Ustadi wa Lugha ya Kiingereza | |
|---|---|
| **Kuanza** | Wanafunzi wa awamu ya kuanza wanaanza kujifunza Kiingereza. Wanaweza kusema lugha moja au zaidi mbali ya Kiingereza na wanaweza kuwa na kiwango kinacholingana na umri cha ujuzi wa maandishi katika lugha yao ya kwanza. Wanafunzi hawa wanaanza kushiriki na shughuli rahisi za lugha za mtaala. |
| **Kujitokeza** | Wanafunzi wa awamu ya kujitokeza wana ujuzi unaokua wa Kiingereza. Wanafunzi hawa wanaweza kusema lugha moja au zaidi zikiwemo Kiingereza cha msingi, na wana ujuzi unaokua wa Kiingereza cha maandishi. Wanafunzi hawa wanaweza kushiriki katika shughuli za darasani na kujihusisha kwa kujifunza wakati wanatolewa ufundishaji unaofaa wa lugha na muda wa ziada wa kukamilisha shughuli za darasani. |
| **Kuendelea** | Wanafunzi wa awamu ya kuendelea wanaweza kusema lugha moja au zaidi, zikiwemo Kiingereza cha matumizi ya kawaida, na wana ujuzi unaokua wa Kiingereza cha maandishi. Wanafunzi hawa ni washiriki hai katika utaratibu wa darasani na shuleni, na wanaweza kujihusisha na kazi za kujifunza na mafanikio ya kuongezeka. Lugha yao ya kwanza inaendelea kuwa msaada muhimu huku wakiendeleza udhibiti wa sarufi ya Kiingereza na kujenga msamiati wao. |
| **Kuimarika** | Wanafunzi wa awamu ya kuimarika wanaweza kusema lugha moja au zaidi, zikiwemo Kiingereza na wana ujuzi mzuri wa Kiingereza cha maandishi. Wanafunzi hawa ni washiriki huru katika utaratibu wa darasani na shuleni, na wana uwezo wa kuongezeka wa kutumia Kiingereza kujihusisha katika kujifunza kwa mafanikio ya jumla. Wanaelewa na kutoa jumbe za mazungumzo na maandishi kwa madhumuni mbalimbali lakini bado wanahitaji ufundishaji na mikakati ya lugha kwa umakini wanaosaidia wanafunzi wa EAL/D, kadri lugha ya kitaaluma ya taaluma za masomo inavyoongezeka. |

## Huduma ya Mkalimani wa Simu

Kama unataka maelezo zaidi tafadhali wasiliana na shule. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kuwasiliana na shule, tafadhali piga simu kwenye Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na omba kupata mkalimani katika lugha yako. Mkalimani yule atapiga simu kwenye shule na atakuwepo kwenye simu ili kusaidia na mazungumzo. Hutatozwa gharama kwa huduma hii.